

SEMINA YA KINGA DHIDI YA UGONJWA WA EAST COAST FEVER  
(ECF) MASHUYO/NDIGANA KALI, BAGAMOYO TAREHE 27/28  
OKTOBA 2016.

UTANGULIZI.

Kama nilivyo jitambulisha naitwa Nicholaus Gideon Kidenke, Mfugaji/Mkulima/Mfayabiashara pia ni Katibu wa Chama cha Wafugaji Kijiji cha Rwakaremera (CHAWAKIRWA) na Mwakilishi wa Wafugaji wa Ngara kwenye Chama Cha Wafugaji Kanda ya Ziwa (CHAWAKAZI) naishi Ngara mjini, Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera.

Katika ufugaji tunaoufanya tunasumbuliwa na magonjwa mbalimbali ambayo tunakabiliana nayo kwa kushirikiana na Wataalamu wetu wa Mifugo. Lakini kuhusiana na ugonjwa huu wa ECF(EAST COAST FEVER) au MASHUYO au NDIGANA KALI tuliuhamu siku nyingi isipokuwa tulikuwa tunakabiliana nao kwa kuogesha ng'ombe kwa kutumia pampu kila wiki pamoja na kutibu kwa dawa aina ya Parvexon au Butalex kwa kuchanganya na dawa saidizi kama tulivyokuwa tunashauriana/Kutibiwa na Wataalamu wa Mifugo.

Pamoja na jitihada hizo za kuogesha na kutibu bado tulijkuta vifo vinaongezeka, ndipo tulimwita Mtaalamu wa Mifugo ili kuchuchunguza vyanzo vya vifo kwa Ng'ombe zetu; Baada ya kupasua Ng'ombe kadhaa ilibainika vifo vilitokana na ugonjwa wa ECF.

Mtaalamu alitushauri mbali na kuogesha/kutibu ipo chanjo madhubuti dhidi ya ugonjwa huo ambapo ndama akichanjwa itamkinga kwa maisha yake yote lakini pia itasaidia kupunguza matumiza ya dawa za kuogesha ng'ombe zetu na inapatikana Dar es salaam Kampuni ya RONHEAM CO. LTD.,

Mimi pamoja na wafugaji wenzangu ambao niliwahamasisha tulianza kuchanja Mwezi Mei, 2013 hadi sasa na kwa kipindi chote hicho binasfi nimechanja ng'ombe 573 yaani mitamba 200 na ndama 373 na bado msimu huu mimi pamoja na wafugaji wenzangu tunatarajia kuchanja chanjo hii

#### CHANGAMOTO

Maeneo ya Malisho na mbegu za malisho

Dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo si za uhakika

Dawa nyingi haziwaui kupe (Taja mfano)

#### RAI YANGU KWA WAHUSIKA

Tunaomba chanjo hii ya ECF itufikie kwa gharama tutakayoimudu wafugaji wengi

Tusaidiwe upatikanaji wa mbegu bora za malisho Kama tulivyomsikia Mh. Waziri (Dkt. Charles Tizeba) kwenye vyombo vyaa habari-TBC (HEKTA MOJA YA MALISHO KULISHA NG'OMBE 60)

#### **ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**